



# do **1** thing

*Misheni ya Do 1 Thing ni kuwahimiza watu, familia, biashara na jamii kujiandaa kwa hatari zote na kuweza kukwepa msiba.*

**LENGO:** Hakikisha kila mtu katika kaya yako anaweza kupokea, kuelewa, na kushughulikia maelezo yaliyopokewa wakati wa dharura.

## Matoleo ya Dharura

Wakati wa dharura, furushi ndogo lenye vitu muhimu vya dharura litafanya hali yoyote kuwa rahisi kushughulikia. Furushi hili linaweza kutengenezwa kwa hali tofauti kulingana na kile wewe na famili yako inahitaji ili kuponea hali ya dharura.

**Chagua moja kati ya mambo yafuatayo ya kufanya mwezi huu ili ujiandae vyema:**

**Kusanya matoleo yako ya dharura katika eneo linaloweza kufikiwa.**

Kuwa na mkoba wa kubeba kama itabidi ujifiche mahali au kuhama nyumbani mwako. Mkoba wako wa kubeba ni sehemu ya furushi lako la dharura la saa 72, hakikisha ni mkoba au kontena rahisi kubeba na nirahisi kuifikia.

### **Fikiria kuhus vitu hizi kwenye mkoba wako wa kubeba:**

- Redio inayowezeshwa na betri na betri za ziada
- Tochi yenye betri za ziada
- Blanketi nyepesi
- Maelezo ya dharura, pamoja na sera za bima
- Orodha ya dawa na matumizi sahihi, na majina ya daktari
- Vitu vya kibinafsi kama vile miswaki, sabuni, miwani ya ziada, n.k.
- Firimbi
- Furushi la huduma ya kwanza
- Mavazi ya kubadilisha
- Kumbwe zisizoharibika
- Vitabu, kadi au magazeti ya kupoteza wakati

## **Pamoja na misingi kwenye ukurasa uliopita, fikiria husu vitu hivi kwenye mkoba wako wa kubeba:**

### *Kwa watoto wadogo:*

- Fomula ya watoto na chakula
- Nepi
- Vipanguzaji vya watoto
- Blanketi au sesere

### *Kwa hali za kimatibabu:*

- Chupa tupu za tembe au orodha ya dawa za sasa\*
- Namba ya simu ya daktari wako

### *Kwa wanyama kipenzi:*

- Chakula na maji ya mnyama kipenzi
- Kola yenye lebo za kutambulisha
- Dawa za wanyama kipenzi
- Vibebea wanyama kipenzi na kamba
- Rekodi za matibabu kutoka kwa hospitali ya wanyama
- Picha ya mnyama wako kipendwa
- Maelezo ya Microchip

\*Hakikisha unasasisha mkoba wako wa kubeba wakati dawa zako zinapobadilika.



## **Unda furushi la matoleo ya dharura la mnyama wako kipendwa, gari lako, na eneo lako la kazi au shule.**

Misiba inaweza kutokea ukiwa mbali na nyumbani. Kama ofisi au shule yako haina furushi la dharura, jitolee kutengeneza moja.

Furushi linapaswa kujumuisha: matoleo ya huduma ya kwanza, ramani za jengo zikionyesha maeneo ya kuhama na kujilinda, tochi, ishara zenye neno la "Ninahitaji Msaada" na "Hakuna Mtu", taratibu za dharura za jengo, ubaoklipu wenye majina ya darasa/wafanyi kazi, na kalamu na penseli.

Tengeneza au nunua furushi la dharura la gari lako. Kama unasafiri na mnyama wako kipenzi mara kwa mara, hakikisha pia kwamba una furushi lake la dharura. Baadhi ya vitu vya kufikiria vya furushi la gari lako ni: furushi ndogo la huduma ya kwanza, tochi, pia za kuangaza, blanketi, chaja ya simu ya mfukoni, kebo kuwasha gari, maji ya chupa, kumbwe zisizo haribika na bendera ya "msaada" au vazi angavu ambalo linaweza kufungwa kwenye antena.



## **Weka pesa kiasi iwapo mitambo ya ATM na ya kadi ya mkopo haiwezi kutumika wakati wa msiba.**

Mambo mengi ambayo sisi hupuuza hayapatikani wakati hakuna umeme. Huenda mitambo ya ATM isifanye kazi. Maduka ya mboga na biashara zingine huenda zisikubali kadi yako ya mkopo au ya matumizi. Pesa taslimu ndiyo inaweza kuwa njia ya pekee ya kununua. Wataalamu wengine wanasema unapaswa kuwa na pesa zisizopungua \$150.00 zilizowekwa kando. Kupata hii huenda isiwezekana kwa kila mtu, kiwango chochote ni kizuri cha kuanza nacho. Chukua dola \$1.00 kila wiki na uiweke katika bahasha katika furushi lako la dharura. Kwa muda mfupi, utakuwa na pesa kiasi zilizowekwa kando kwa matumizi wakati wa dharura.



*Wakati hali kali ya hewa imetabiriwa, hakikisha gari lako limejaa mafuta. Hutaki kusubiri kwenye mstari kwa ajili ya mafuta ukiambiwa uhame. Dhoruba zingine huenda zikapoteza umeme, kwa hivyo kufanya vituo vya mafuta kufunga.*